CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

# MATUKIO YA MWEZI

JANUARI NA FEBRUARI, 2020












*"ARDHI NI HAZINA"*

# SUA yakabidhiwa rasmi Majengo Katavi



Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Mizengo Pinda na Mkuu wa Chuo Kikuu cha SUA Jaji Mstaafu Mhe. Joseph S. Warioba wakiweka saini ya makubaliano ya kukabidhiwa majengo hayo kwa SUA

Chuo kikuu Cha Sokoine Cha kilimo SUA kimekabidhiwa rasmi ardhi na majengo ya Kampasi ya Mizengo Pinda Mkoani Katavi ambapo Viongozi mbalimbali waliozungumza katika hafla ya makabidhiano wamesema ujio wa Chuo hicho Cha kilimo ni fursa ya mabadiliko kwa Mikoa ya nyanda za juu kusini inayoongoza kwa uzalishaji wa chakula nchini lakini ingali Bado ikitajwa katika takwimu za kitaifa kuwa na changamoto ya udumavu na umasikini.

Wakati wa hafla hiyo Waziri Mkuu Mstaafu Mh. Mizengo Pinda ambaye ndiye aliyekuwa Mmiliki wa awali wa ardhi hiyo na Majengo aliyojengewa na Wahisani amesema kulikuwa na malengo mengi ya matumizi ya majengo hayo ikiwemo kuwa shule ya msingi au chuo Cha afya lakini lengo la kuwa chuo Cha kilimo limeakisi hasa maana halisi ya ukanda wa eneo husika kwa kuwa wakazi wengi wanajishughulisha na kilimo,uvuvi na ufugaji.

Aliongeza kuwa uwepo wa chuo Cha sua katika eneo hilo majengo hayo yatatumika kwa nia pana kuliko walivyofikilia na kutakuwa na ongezeko la fursa za kimaendeleo na thamani ya mkoa kuelekea kuchangia pato la taifa na kutokomeza alichokiita laana kwa baadhi ya mikoa ikiwemo Katavi kutajwa katika takwimu za taifa za umasikini na udumavu utapia mlo huku kukiwa na uzalishaji mkubwa wa chakula. Waziri mkuu huyo mstaafu alikiomba chuo kikuu Cha




Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda (wa pili kushoto) akiwa na Baadhi ya Wadau walioshiriki kwenye Hafla ya kukabidhi Majengo ya Kampasi ya mizengo Pinda Mkoani Katavi

***Inatoka ukurasa wa pili***

sokoine Cha kilimo sua miongoni mwa vitu vya haraka vya kusaidia jamii kwa kuanza iwe kutoa elimu kwa wakazi wa vijini vya jirani juu ya kuondokana na udumavu na umasikini pamoja na elimu ya ujasilimiamali hasa kwa vijana kwa kuwa anaamini sua ndio mkombozi wa jawabu la kutoa mkoa huo katika takwimu hizo na kuongeza fulsa za kimaendeleo huku akiwataka wakazi wa katavi hasa wa vijiji vya jirani kuchangamkia fulsa zitakazokuwepo na siyo kuja kulalamika baadae.

Kwa upande wake mgeni rasmi katika hafla hiyo ya makabidhiano ya ardhi na majengo Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mh.Joyce Ndalichako aliwashukuru sua kwa kuwa wepesi kukubali ombi la kuwa na campus hiyo na kuwa na utekelezaji wa haraka na ameagiza chuo Sasa kifanye haraka taratibu za kupata ithibati kutoka tume ya vyuo vikuu Tanzania (TCU) ili kiruhusiwe kuanza udahili wa wanafunzi mwaka huu wa masomo 2020-2021.

"Chuo hiki ni fulsa nyingine kwa vijana wa kitanzania katika misitu, mifugo na kilimo tena kiko mahala sahihi, wanakatavi sote na kwa Umoja wetu wakiwemo wajasilimiamali tuchangamkieni fulsa, asiwepo wa kubaki nyuma kila mmoja wetu aangalie uwepo wa anachoweza kufanya kwa ajili ya kujikwamua"

Nae mkuu wa chuo Cha sokoine Cha kilimo Sua aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa kwanza wa Rais Mstaafu Jaji Joseph Sinde Warioba alisema tangu kupata kwa Uhuru wakulima wadogo wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali pamoja na uwepo wa sera hivyo kuongezeka kwa mizengo pinda campus kutasaidia wakulima wa nyanda za juu kusini kulima kwa tija na kuondokana na kilimo Cha mazoea.

Kufuatia kutoa eneo Hilo na majengo kwa sua Warioba alisema

"Pinda ni kijana wangu watu walikuwa wanapenda kumuita mtoto wa mkulima Sasa umepata promotion utakuwa uanitwa mkulima kamili kupitia uamuzi wako wa kutoa eneo kuwa chuo Cha kilimo"

Kwa upande wake makamu mkuu wa chuo Cha sokoine Cha kilimo sua Prof. Raphael Chibunda alianza kwa kutoa historia fupi ya kuanzishwa kwa chuo kikuu Cha Sokoine Cha Kilimo Sua na namna alivyopokea wito kutoka kwa Mkuu wa Mkoa Katavi Mh. Juma Homera kwamba Waziri Mkuu Mstaafu Mh. Mizengo Pinda anamtafuta na walipokutana alimweleza nia yake na uongozi wa wilaya na mkoa kuyatoa majengo hayo kwa sua.

Aliongeza kuwa michakato mbalimbali iliendelea ikiwa ni pamoja na baraza la chuo kulidhia kuanzishwa kwa campus mpya ya mafunzo katika Mkoa wa Katavi kwa ajili ya kutoa mafunzo ya shahada za awali na shughuli za utafiti waugavi ikiwa pamoja na mabadiliko ya bajeti ya chuo ili kukiwezesha chuo kutenga zaidi ya sh milioni 330 ili zitumike katika kuboresha baadhi ya miundombinu na shughuli za awali za kituo.



*"Chuo hiki ni fulsa nyingine kwa vijana wa kitanzania katika misitu, mifugo na kilimo tena kiko mahala sahihi, wanakatavi sote na kwa Umoja wetu wakiwemo wajasilimiamali tuchangamkieni fulsa, asiwepo wa kubaki nyuma kila mmoja wetu aangalie uwepo wa anachoweza kufanya kwa ajili ya kujikwamua"*

***"ARDHI NI HAZINA"***

# Wakulima watumieni Wawekezaji kuinua ujuzi na maarifa katika Kilimo- Prof. Chibunda



*Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda akiwa katika moja ya Shamba la Mahindi lililo chini ya Mradi wa "Farm For The Future"*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA kimesema ili nchi ya Tanzania iendelee katika sekta ya kilimo juhudi za makusudi zinahitajika katika kuhakikisha wananchi wanachukua jukumu la kujiletea maendeleo kwa kubadilisha aina ya kilimo na kufanya kiwe cha kibiashara kwa kutumia mbinu bora za kilimo yaani kuzipokea na kuzitumia mbinu za wawekezaji wenye nia ya kuikwamua jamii katika changamoto mbalimbali

Hayo yamesemwa February 18, 2020 Ilula mkoani Iringa na Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Prof. Raphael Chibunda wakati wa ziara ya siku moja ya kutembelea uwekezaji katika kilimo biashara unaofanywa na "Farm For the Future"



*Prof. Raphael Chibunda (kushoto) akizungumza jambo na Mmoja wa Wamiliki wa Mradi Bw. Osmund Ueland (kulia)*

Prof. Chibunda ambaye katika ziara hiyo aliambatana na viongozi na wataalam mbalimbali kutoka SUA amesema wananchi katika maeneo mbalimbali nchini kama watatumia mbinu bora za kilimo na kukubali kuasili mbinu zinazotumiwa na wawekezaji wakubwa wanaweza kuwa na uzalishaji wenye tija ambao utainua maisha yao na wataweza kujiletea maendeleo kwani wapo wawekezaji ambao wana nia ya dhati ya kutaka kusaidia jamii

Makamu huyo wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo aliongeza kuwa SUA itaendelea na kazi ya kuhakikisha inawafikia wakulima katika maeneo yao kwani hivi sasa inaangalia uwezekano wa kushirikiana na mwekezaji huyo ili kutumia shamba hilo katika mafunzo na tafiti kwa wanafunzi wake na matokeo ya tafiti hizo yatanufaisha wakulima wote nchini kama ambavyo imekuwa ikisisitizwa Rais Mhe. Dkt John Pombe Magufuli

# SUA yachangia utatuzi wa ajira kwa vitendo



Naibu waziri wa kazi ajira na vijana Mh. Antony Mavunde akisisitiza jambo wakati wa hafla ya kukabidhi tiketi kwa vijana wanaokwenda Marekani kwa Mafunzo

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA kimepongezwa kwa kuwa chuo kinachotoa mchango mkubwa wa utatuzi wa ajira kwa vitendo na kilichofanikiwa kuwabadilisha fikra vijana wahitimu wa vyuo vikuu nchini.

Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Vijana Mh. Antony Mavunde ameyasema hayo wakati akikabidhi tiketi kwa vijana 12 wahitimu wa SUA wanaokwenda nchini Marekani kupitia programu ya mafunzo kwa vitendo kwa wanachama wa SUGECCO.

Alisema uwepo wa SUA kwa miaka ya hivi karibuni unaonekana kwa vitendo hasa katika kutatua changamoto ya ajira kwa Vijana na uthubutu wa chuo hicho kuwabadili vijana kifikra hali inayowafanya vijana hao kuwaza kujiajiri kupitia kilimo kutokana na mafunzo wanayopata wakiwa chuoni.

Naibu Waziri huyo aliwaasa Vijana wanaokwenda Marekani kuhakikisha wanakuwa mabalozi wazuri wa chuo cha SUA na Tanzania kwa ujumla na kurudi na ujuzi wenye tija kwa Taifa.

Kwa upande wake Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha kilimo SUA Prof. Raphael Chibunda aliishukuru serikali ya awamu ya tano kwa kuleta fedha za maendeleo chuoni pamoja na kuihakikishia serikali kuwa SUA itaendelea na program mbalimbali ambazo zitaendelea kuleta tija kwa Taifa.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma Prof. Peter Gillah alitoa pongezi kwa SUGECCO kwa kuanzisha program hiyo ya mafunzo ya kuwapeleka vijana katika nchi mbalimbali na kuwaasa vijana wanaosafiri kuhakikisha wanarudi na maarifa tofauti yatakayoleta chachu kwa vijana na mabadiliko nchini katika sekta ya kilimo.



Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (Taaluma) Prof. Peter Gillah akiongea jambo wakati wa hafla ya kukabidhi tiketi kwa vijna hao

# Naibu Spika awataka Wanafunzi wa kike kujifunza toka kwa watu waliofanikiwa




***Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Tulia Ackson akiongea na washiriki wa Semina ya Wanafunzi wa Kike kuhusu Msichana mwenye Malengo***

Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Tulia Ackson amewataka wanafunzi wa kike kujifunza kwa kufanya mambo na kuishi maisha wanayoishi watu waliofanikiwa ili kuweza kutimiza ndoto zao na kulisadia Taifa.

Wito huo ameutoa wakati akifungua semina ya Wanafunzi wa kike wanaosema Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA na wengine kutoka vyuo mbalimbali vya Mkoani Morogoro iliyo huru msichana mwenye malengo.

" Kama unataka kuwa Mwalimu wa Chuo jifunze na msikilize Mwalimu wa Chuo anavyofundisha na jifunze kwake, kama unataka kuwa Kiongozi mkubwa basi jifunze kwa kiongozi unayetamani kufanana nae kwenye maisha hivyo lazima myaishi maisha mnayotaka kutaishi huko baadae" Alisema Mhe. Tulia.

Aliongeza kuwa anajua chuoni kuna ni sehemu huru ambayo hakuna anayewafuatilia kama ilivyokuwa shule za sekondari lakini ni lazima wahakikishe wanatumia uhuru huo kufanya mambo ya msingi na yenye tija kwao na kuhakikisha wanatimiza lengo lao kuwa chuoni hapo.

Mhe. Tulia aliongeza kuwa anajua vyuoni wasichana na wavulana wanakuwa kwenye mahusiano kutokana na mazingira hayo lakini wavulana wanafaulu kwakuwa wanasoma na wasichana wanafeli kutokana na kutumia muda wao kuwapikia na kuwahudumia wapenzi wao ili wakitoka darasani wale.



***Washiriki wakisikiliza kwa umakini neno toka kwa Naibu Spika Mhe. Tulia ACKSON***

# SUA yatajwa kuwa kitovu cha utafiti nchini



*Picha ya pamoja kati ya Viongozi wa SUA pamoja na baadhi ya Wajumbe toka Chuo cha Taifa cha Ulinzi*

Mkurugenzi wa Mafunzo Chuo cha Taifa cha Ulinzi Bi. Lucy Shule amesema kuwa Chuo cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ni kitovu cha tafiti mana tafiti nyingi zinaonekana kufanyika SUA na wataalamu mbalimbali, utafiti ni kitu cha msingi ambacho mtu anatakiwa kufanya awe na maendeleo yake mwenyewe.

Bi Lucy Shule amesema hayo mara baada ya kumalizika kwa Ziara ya kutembelea SUA iliyokuwa inakamalisha sehemu ya mafunzo yao kwa vitendo kwa wanafunzi waliotoka Chuo Cha Taifa cha Ulinzi kilichopo mkoani Dar es salaam na ziara iliyofanyika leo tarehe ya 17 Januari 2020, Kampasi Kuu - SUA.

Alizungumza kuwa wanafunzi wamemaliza somo la kwanza la mafunzo ambalo walikuwa wanasoma kwa nadharia na wamekuja huku kuja kujifunza kwa vitendo kuona vile ambavyo walikuwa wamejifunza.

“Tumechagua kuja SUA ni sehemu ya mafunzo kwa vitendo washiriki wetu wa kozi wanafanya masomo yanayohusiana na usalama wa Taifa na strategia na unapozungumzia usalama wa Taifa na Strategia ni kitu ambacho kinachojumuisha sekta zote ingawaje mwanzoni ilikuwa inaonekana ni swala Zaidi linalohusu vyombo vya ulinzi na usalama peke yake lakini ukiangalia Zaidi kwa mapana yake kwa usalama wa Taifa inajumuisha maswala ya kiuchumi na unaposema uchumi kuna kilimo,ufugaji, uvuvi, umwagiliaji“ alisema Bi. Shule

Kwa upande wa mshiriki wa mafunzo wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi Bw. Athumani Hussen alisema SUA ni miongoni mwa Chuo cha Kilimo Nchini na Kilimo ni eneo mojawapo linalochangia maendeleo ya Taifa, Maendeleo ya Taifa ni jambo mojawapo linalowezesha usalama wa Nchi mfano usalama wa chakula unapatikana kwa matokeo ya tafiti za SUA.

Nae Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Utawala na Fedha Prof. Hyasinta Muzanila alisema kuwa Chuo cha Sokoine cha Kilimo kimefurahi kutembelewa na wanafunzi na Walimu wa Chuo cha Ulinzi cha Taifa na kwa kuchagua SUA inaonesha kwamba wanakitambua na kujua umuhimu wa kazi zinazofanyika Chuoni, pamoja na Mafunzo yanayotolewa hasa kwa utafiti na kuweza kuona kuwa ni mchango mkubwa kwa wao kujifunza.

Alisema kutokana Na hii ziara itapelekea Chuo kutangazwa hadi nje ya Tanzania sababu baadhi ya wanafunzi wa Chuo cha Ulinzi cha Taifa wanatoka nchi mbalimbali na wakirudi makwao watakiongelea SUA kwa uzuri na mapana zaidi na watu wengi watakifahamu Chuo.

# SUA na Chuo Kikuu cha BANAT kubadilishana uzoefu



*Makamu wa Mku wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda (wa nne kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi toka Chuo cha BANAT na baadhi ya Viongozi toka SUA*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Chuo Kikuu cha Sayansi za Kilimo na Tiba za Mifugo cha nchini Romania BANAT vimesaini makubaliano ya awali ya kushirikiana katika kubadilishana uzoefu wa Kitaaluma hasa upande wa Kilimo.

Makubaliano hayo ya awali yamefanyika tarehe 11 Februari 2020 katika Kampasi Kuu ya SUA ambayo yamemuhusisha Makamu Mkuu wa Chuo cha BANAT Prof. Sorin Stanciu, Naibu Mkuu wa Ndaki ya Kilimo Dkt. Laura Smuleac na Mkurugenzi Dkt. Raul Pascalau anayehusika na Masuala ya Ushirikiano wa Nje ya nchi ya Romania na Viongozi kutoka SUA akiwemo Makamu wa Mkuu wa Chuo hicho Prof. Raphael Chibunda

Akizungumza mara baada ya kusaini makubaliano hayo Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Uzamili, Utafiti na Uwasilishaji wa teknolojia na ushauri wa kitaalam Prof. Esron Karimuribo alisema lengo la viongozi kuja SUA ni kuanzisha ushirikiano ambao utajikita katika kuboresha mahusiano ya kitaaluma kati ya wanataaluma na wanafunzi kutoka Chuo cha SUA na Chuo cha BANAT.

Prof. Karimuribo alisema vyuo hivyo viwili vinafanana sana kwani wao wana ndaki tano ikiwemo Ndaki ya Kilimo, Ndaki ya Tiba na Mifugo, Ndaki ya Chakula na Ndaki ya Maendeleo ya Wananchi hasa upande wa vijijini hata programu za kufundishia zinafanana sana na za kwetu.

Alisema kuwa chuo cha batan kinatoka nchini Romania ambako kuna hali ya hewa ya baridi na Tanzania iko kwenye nchi zenye hali ya hewa ya joto hivyo ushirikiano wetu ni fursa ya kujifunza zaidi jinsi ya kuendesha kilimo kwenye ukanda wa baridi na ukizingatia na sisi tuna mikoa ambayo ina hali ya hewa ya baridi kama vile Mbeya, Iringa, Arusha na Kilimanjaro na wao pia watajifunza jinsi ya kuendesha kilimo kwenye nchi zenye joto.

"Chuo chao kina zaidi ya miaka 50 katika kuendesha mafunzo na taaluma hivyo sisi kupeleka wanataaluma wetu kule na wanafunzi watajifunza mbinu nzuri zaidi za kuendeleza taaluma ya kilimo watakaporudi Chuoni" alisema Prof. Karimuribo

# Vijana watakiwa kuchangamkia fursa za Ujasiriamali



*Rasi wa Ndaki ya Sayansi za jamii na Insia Dkt Samwel Kabote akielezea jambo mara baada ya kumalizika kwa Warsha ya mpango wa kuendeleza wajasiriamali vijana na Wavumbuzi Tanzania*

Watanzania hususani Vijana wametakiwa kujitokeza na kuchangamkia Miradi, Mafunzo na Fursa zozote ambazo zimejikita katika kuwajengea uwezo Wajasiriamali kutokana na eneo hilo kuwa muhimu katika kuongeza ajira, maendeleo ya Jamii na kuinua uchumi wa taifa.

Ushauri huo umetolewa na Rasi wa Ndaki ya Sayansi za Jamii na Insia Dkt Samwel Kabote wakati wa Warsha ya mpango wa kuendeleza Vijana Wajasiriamali na Wavumbuzi Tanzania hususani vijana wa kike iliyofanyika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo – SUA, Januari 29, 2020 iliyowakutanisha vijana walio kwenye program ya mafunzo ya ujasiliamali kutoka Tanzania,Kenya Uganda na Marekani.

Dkt. Kabote aliesema kuwa taarifa iliyotolewa na Shirika la kazi Duniani (ILO) Mwaka 2017 inaonesha kuwa asilimia 12.7 ya Watanzania walikuwa hawana Ajira hivyo kama Chuo wamekuwa na jitihada binafsi za kuweza kuanzisha ushirikiano na Vyuo vingine Duniani Katika utoaji wa Mafunzo ya Ujasiriamali hususani kwa vijana wa kike ili kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira.



# Kamati ya kuthibiti uadilifu SUA yajipanga kusimamia uadilifu



Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (Utawala na Fedha ) Prof. Hyasinta Muzanila (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wa Kamati ya Uadilifu ya SUA

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA, kimewataka wanafunzi, wafanyakazi na wanajumuiya wa SUA kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa Kamati ya Kuthibiti Uadilifu KKU iliyopo SUA ili kuhakikisha kila mwanafunzi na mfanyakazi katika taasisi hiyo anawajibika kwa kufanya kazi kwa uadilifu, kuepuka rushwa na matendo mbalimbali ya uonevu.

Hayo yamesemwa Februari 15, 2020 na Naibu Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Utawala na Fedha, Prof. Yasinta Muzanila wakati akifungua mafunzo kuhusu Kamati ya Kuthibiti Uadilifu kwa viongozi mbalimbali wa Serikali ya wanafunzi SUASO na wawakilishi wa madarasa iliyofanyika chuoni hapo

"Serikali yetu hii ya awamu ya 5 inayo mikakati mingi ya kuboresha utawala bora na mkakati mmoja wapo ni kuthibiti uadilifu pia kuthibiti rushwa, na kama tunavyofahamu kwamba rushwa ni adui wa haki na si kwa Tanzania tu bali Ulimwengu mzima" alisema Prof. Muzanila

Naye Mwenyekiti wa KKU chuoni hapo Prof. Christopher Mahonge alisema kamati imeandaa mpango kazi wa mapambano dhidi ya rushwa, kupokea, kuchambua na kushughulikia malalamiko toka ndani na nje yanayotokana na ukiukwaji wa maadili

"Lakini pia kamati itashiriki katika kutoa mafunzo kuhusu maadili, utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa kwa maafisa wa ngazi za kati, mameneja na watumishi wa kawaida" alisema Prof. Mahonge

Prof. Mahonge aliongeza kuwa taasisi za serikali ikiwemo SUA zinao wajibu mkubwa wa kuhakikisha zinatoa huduma bora na kuzingatia masilahi ya umma na thamani ya fedha inayotumika katika huduma hizo hivyo ni muhimu kwa kila mtu kuwajibika

Akizungumzia mafunzo hayo Rais wa Serikali ya Wanafunzi SUA Bw. Mbalamwezi Hussein Ismail alisema hivi sasa suala la uadilifu limekuwa changamoto kubwa kwa watanzania kwa hiyo mpango huu wa Serikali utawaweka watu kuwa na ufahamu juu ya masuala ya rushwa na uonevu

Naye Waziri Mkuu wa Serikali ya wanafunzi SUA Bi. Jenipher Karoli Tairo amesema jambo hili litasidia wanafunzi kusoma katika mazingira rafiki ambayo yatawasaidia katika masomo yao

"Uadilifu unaposimamiwa katika mazingira ya shule hakika wanafunzi watasoma katika mazingira ambayo ni rafiki kwa maana ninaamini hakutakuwa na bugudha kutoka kwa waalimu hususani kwa wanafunzi wa kike" alisema Jenipher

# Uadilifu na Uwajibikaji ndio nyezo muhimu mahala pa kazi




*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo cha SUA Utawala na Fedhja Prof. Hyasinta Muzanila (aliyesimama) akiongea na Washiriki wakati akizindua rasmi Semina ya Chama cha Wafanyakazi Taasisi za Elimu ya juu (THTU)*

Uadilifu na Uwajibikaji kwa Watumishi wa umma mahala pa kazi ndio nyenzo muhimu na njia sahihi ya kutatua changamoto mbalimbali zinazowakumba Watumishi wa umma.

Hayo yamebainishwa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (Utawala na Fedha) Prof. Hyasinta Muzanila kwa niaba ya Mgeni rasmi ambaye ni Makamu Mkuu wa Chuo Prof Raphel Chibunda wakati wa uzinduzi wa Semina Maalumu ya Chama cha Wafanyakazi Taasisi za Elimu ya juu (THTU) Tawi la SUA iliyofanyika siku ya Jumanne Tarehe 25 Februari 2020 katika Darasa la MLT2 Chuoni hapo.

Alisema kuwa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kinatambua umuhimu wa mchango wa Vyama vya Wafanyakazi mahala pa kazi hasa katika kudai na kutetea masilahi ya Wafanyakazi.

Alisema kuwa kwa kulitambua hilo na umuhimu wake mkubwa SUA imeendelea kufanya kazi pamoja na Vyama hivyo vya Wafanyakazi kwa pamoja ili waweze kutatua changamoto mbalimbali zinazo wakabili Watumishi katika Chuo hicho na mara kwa mara kumekuwa na mikutano kadha wa kadha ili kwa pamoja waweze kusaidiana kukifanya Chuo kiweze kusonga mbele.

"Naomba nikili wazi kuwa THTU hapa SUA haijafanikiwa kuwa bargaining trade union lakini Chama hiki kimekuwa mstari wa mbele katika kupigania na kudai

Inatoka ukurasa wa 11

## Uadilifu na uwajibikaji ndio nyezo muhimu mahala pa kazi

haki za Watumishi hapa SUA na mara kadhaa Viongozi wake wamekuwa wakifika katika ofisi zetu ili kutukumbusha mambo mbalimbali ambayo ni muhimu na yanayohuu ustawi wa Chuo pamoja na watumishi wake kwa ujumla" alisema Prof Muzanila

Aidha alisema kuwa THTU imebaini kuwa migogoro mingi inayowafikia toka kwa Wafanyakazi mara nyingi chimbuko lake limekuwa ni kwamba Watumishi walio wengi wanafanya kazi chini ya kiwango stahiki cha uadilifu na wengine uwajibikaji wao unakuwa ni hafifu.

Nae Mkurugenzi Mkuu kitengo cha kukuza maadili katika huduma za umma ofisi ya Rais utumishi wa umma na utawala bora na maadili utumishi wa umma Ndugu Fabian Pokela alisema kuwa uadilifu na uwajibikaji ni vipa umbele muhimu katika kufikia malengo ya taasisi yeyote kama Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na taifa kwa ujumla.

"Taasisi nyingi Serikalini zinaporomoka na kuharibika na kutofikia malengo sio kwa sababu bajeti ni ndogo ila ni kwa sababu watumishi wake wamesahau kuwa uadilifu na uwajibikaji ndio silaha muhimu katika kufanikiasha malengo ya taasisi husika" alisema Ndg. Pokela

Alisema kuwa Uadilifu mahala pa kazi sio tu kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na Mamlaka husika bali pia ni kuwa na hofu ya Mungu kwani tunatambua kuwa Mungu ndiye Muadilifu Mkuu na ameweka Sheria ndani yetu.



*Baadhi ya Watumishi wa SUA wakisikiliza jambo kwa umakini wakati wa Semina maalumu ya Chama cha Wafanyakazi Taasisi za Elimu ya juu*

# Wanajumuiya SUA washauliwa kushiriki mihadhara na warsha


Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) Prof. Lazaro Busagala akifafanua jambo kuhusu faida za teknolojia ya Nyuklia na Mionzi wakati wa Mkutano wa hadhala SUA

Wanajumuiya wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA wameshauliwa kuwa na tabia ya kushiriki kwenye Warsha na Mihadhara ya wazi inayohusisha utoaji wa Elimu juu ya Kilimo na Mifugo kwa kuwa Chuo hicho ndio kitovu na Mdau mkubwa wa maswala mbalimbali ya Kilimo nchini.

Kauli hiyo Imetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) Prof. Lazaro Busagala wakati wa muhadhara wa wazi juu ya matumizi salama ya Teknolojia ya Nyukria na udhibiti wa Mionzi uliofanyika siku ya Jumanne Tarehe 18 Februari 2020 katika ukumbi wa madarasa mapya ya chuo (New Lecture Theatre).

Alisema kuwa wao kama Tume wamekuwa wakifanya Mihadhara na kutoa Elimu juu ya matumizi salama ya Teknolojia ya nyuklia na udhibiti wa mionzi katika Vyuo Vikuu nchini kwa kuwa wao ndio Wadau wakubwa na Washirika wao wa karibu husussani Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA, hivyo anaamini wakati mwingine Wanajumuiya wa SUA watajitokeza kwa wingi kwani Teknolojia hiyo ina faida nyingi katika masuala ya kilimo na ufugaji.

Aidha aliongeza kuwa, kwa upande wa SUA Teknolojia hiyo inatumika sehemu mbalimbali kwa mfano katika kuhifadhi chakula, uzalishaji wa Wanyama na pia kwenye kutengeneza mbegu bora.

"Kwa mfano kwa sasa tuna Mbegu ambayo inaitwa Tasiri au kuna nyingine inaitwa super visgule Zanzibar ya mpunga ambayo inazalisha mara mbili zaidi ya mbegu ya kawaida, lakini zote hizo ni faida zinazopatikana na Teknolojia hii ya Nyuklia" alisema Prof. Busagala


Baadhi ya Wadau wakisikiliza mawasilisho kuhusu matumizi salama ya Teknolojia ya Nyuklia na Mionzi

# Vijana waaswa kubadili tabia kujikinga na maambukizi ya ukimwi



Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (Utawala na Fedha) Prof. Hyasinta Muzanila (mwenye kipaza sauti) akisisitiza jambo kwa Washirki wa Semina ya Ukimwi na Magonjwa yanayoambukiza

Vijana hasa wanafunzi wa Elimu ya juu wametakiwa kubadili tabia na mwenendo wao ili Kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI, magonjwa Sugu ya kuambukiza na madawa ya kulevya kutokana na wao kuwa katika hatari zaidi na hivyo kupoteza nguvu kazi ya Taifa.

Hayo yamesemwa na Kaimu Naibu makamu mkuu wa Chuo Utawala na fedha Prof. Yasinta Muzanila aliyemuwakilisha Makamu wa Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chibunda kwenye semina kuhusu UKIMWI na magonjwa yanayoambukizwa iliyoandaliwa na Club ya UKIMWI kwa kushirikiana na Hospitali ya SUA.

Prof. Muzanila amesema vijana wengi ambao wapo kwenye kundi hilo wapo vyuo vikuu na wengine mitaani hivyo wasipo kitambaa na kubadili tabia watapoteza Nguvu kazi ya Taifa na familia zao ambazo zinawategemea.

"Zamani tulikuwa tunasoma vijana ni Taifa la kesho lakini sasa tunaona na kuamini kuwa vijana ni taifa la sasa hivyo ni lazima mpate elimu kuhusu masuala haya ili mjitambue na mjikinge na athari zozote za kiafya maana tunaposema Tanzania ya viwanda tunawategemea vijana katika kutimiza hili" Alisisitiza Prof. Muzanila.

Awali akizungumzia lengo la Warsha hiyo Datari Mkazi wa Idara ya Hospitali ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Dkt. Omary Kasui alisema SUA AIDS club ni sehemu ya Mikakati ya Chuo katika kuzuia maambukizi ya UKIMWI, Magonjwa Sugu ya Kuambukizwa na madawa ya kulevya.

Dkt. Kasui alibainisha kuwa Club hiyo ilianzishwa Mwaka 2000 ili kupambana na maambukizi ya chuoni na inahusisha wananafunzi pamoja na wafanyakazi na wanajumuiya wote katika kutoa elimu na kujikinga na maambukizi hayo.



Daktari Mkazi wa Idara ya Hospitali ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Dkt. Omary Kasui akiongea wakati wa Semina kuhusu Ukimwi na magonjwa yanayoambukizwa

# Wanafunzi wa SUA watakiwa kutumia michezo kuboresha afya zao



Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Wametakiwa kutumia michezo kuboresha afya zao kwasababu mwili wenye afya nzuri hupelekea akili kufanya kazi vizuri.

Hayo yamesemwa na Rasi wa Ndaki ya Solomon Mahlangu ya Sayansi na Elimu Prof. Lewis Malisa kwa niaba ya Makamu wa Mkuu wa Chuo Prof. Raphaeli Chibunda wakati wa ufunguzi wa Michezo ya ndani ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (INTRA-MULAR GAMES) kwenye viwanja vya mpira wa miguu Kampasi ya Solomon Mahlangu – Mazimbu iliyoanza tarehe 21 februari 2020 na inategemewa tamati ya michezo hiyo kuwa mwishoni mwa mwezi wa nne 2020.

"Kwaiyo nategemea kwenye nafasi hii ambayo Wanafunzi mmeipata ya kushiriki michezo mtaitumia vizuri na mwili utakuwa na afya nzuri pia watakaocheza hata matokeo ya mitihani yao watafanya vizuri"alisema Prof. Malisa.

Prof. Malisa aliongeza kuwa michezo ni jambo muhimu sana kwa afya ya binadamu na inatoa fursa ya watu kujuana,kushirikiana katika mambo mbalimbali na kuonyeshana furaha na upendo.

Vile vile aliwaomba wachezaji wote wacheze michezo kwa hekima ya juu na kwa uangalifu mkubwa ili kuepukana kuumizana uwanjani sababu wamekaribia kuingia kwenye mitihani si vizuri mwingine ashindwe kufanya mitihani sababu ya majeraha.

Kwa upande wa Mkuu wa Idara ya Michezo Bw. Masoud John Gumbwa alisema kuwa michezo ya ndani ya wanafunzi wa SUA inahusisha Wanafunzi wa Kampasi Kuu na Kampasi ya Solomon Mahlangu inayofanyika mara moja kila mwaka na mshindi wa kwanza wa mpira wa miguu anapata ngo`mbe na mshindi wa kwanza kwenye michezo mingine anapata mbuzi.